**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 7, Issue 1, 2024**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Usawiri Chanya wa Hadhi ya Mwanamke katika Methali za Igikuria

*Maroa Dunstan Sospeter[1*] na Prof. Catherine Ndungo, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100, Nairobi, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: dunstanmaroa@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2048**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*15 Julai 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Methali, Ufeministi, Utamaduni, Usawiri.*

**IKISIRI**

Makala hii imechunguza usawiri chanya wa hadhi ya mwanamke katika methali za Igikuria. Swala la usawiri wa mwanamke limeshughulikiwa na watafiti wa awali huku tafiti zao zikiibua usawiri hasi wa mwanamke. Tafiti hizi za awali kama za Matteru (1993) na Ndungo (1998) zilifanywa kuhusu vipera vya fasihi simulizi kama vile; nyimbo na methali zilidhihirisha namna tofauti mwanamke anavyodunishwa katika jamii za Kiafrika. Udunishwaji huu unatokana mifumo tawala inayompendelea mwanamume. Mifumo hii imejificha katika mila na desturi potovu za jamii mbalimbali. Aidha, ingawa jamii huweza kumdunisha mwanajamii yeyote yule kwa kutegemea matendo yake, kuna miktadha mbalimbali ambayo humfanya mtu kupata sifa nzuri kulingana na matendo yake mazuri. Mwanamke anapochangia katika shughuli mbalimbali za jamii hupewa sifa si haba. Kutokana na haya, panaibuka haja ya kuchunguza usawiri chanya wa mwanamke katika methali za Igikuria kwa kudhihirisha anavyotukuzwa katika jamii, miktadha inayompelekea kusifiwa na mchango anaotoa katika kuendeleza asasi mbalimbali za kiuchumi, kisiasa, na kijamii. Makala hii imeongozwa na nadharia ya Ufeministi ambayo iliwekewa misingi na Wollstonecraft (1992), Woolf (1929) na Beauvoir (1994). Mihimili ya Ufeministi iliyotuongoza ni usawazishaji wanadamu kwa upande wa utamaduni na uana, utumiaji wa fasihi kama jukwaa la kueleza kwa uyakinifu hali inayomkumba mwanamke ili iweze kueleweka na watu wengi na kuhamasisha watumiaji wa sanaa wawe na wahusika wa kike ambao ni vielelezo wenye uwezo na wanaoweza kuigwa. Data iliyotumika katika Makala hii ilitolewa maktabani na nyanjani. Maktabani, tasnifu, makala na vitabu vinavyohusiana na mada vilisomwa kwa kina. Nyanjani, data ya methali za kumtukuza mwanamke ilikusanywa kwa njia ya hojaji. Uwasilishaji wa matokeo umefanyika kwa njia ya maelezo na michoro faafu. Matokeo yameonyesha kuwa katika methali za Igikuria, mwanamke amesawiriwa kama mfadhili katika ukoo anaotoka, mshauri wa jamii, kiongozi katika shughuli muhimu za jamii (sherehe), mtetezi wa jamii, mlezi, mjenzi wa familia na msingi thabiti katika jamii. Pia mwanamke amejitokeza kuwa chemchemi katika maisha ya Wakuria. Hidaya na uwezo wa kipekee aliotunukiwa mwanamke na Jalali katika kuendeleza jamii kupitia kwa njia ya uzazi, unamfanya kusifiwa kiasi kuwa mji usio na mwanamke hulinganishwa na chaka lisiloingilika. Aidha, miktadha ya kijamii ambayo inapelekea mwanamke kutukuzwa ni ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

sherehe za kitamaduni, shughuli za kilimo na uzalishaji mali, shughuli za uzazi na malezi.

**APA CITATION**

Sospeter, M. D. & Ndungo, C. (2024). Usawiri Chanya wa Hadhi ya Mwanamke katika Methali za Igikuria. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 332-342. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2048.

**CHICAGO CITATION**

Sospeter, Maroa Dunstan and Catherine Ndungo. 2024. "Usawiri Chanya wa Hadhi ya Mwanamke katika Methali za Igikuria". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 332-342. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2048

**HARVARD CITATION**

Sospeter, M. D. & Ndungo, C. (2024) "Usawiri Chanya wa Hadhi ya Mwanamke katika Methali za Igikuria", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 332-342. doi: 10.37284/jammk.7.1.2048

**IEEE CITATION**

M. D. Sospeter & C. Ndungo "Usawiri Chanya wa Hadhi ya Mwanamke katika Methali za Igikuria", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 332-342, Jul. 2024.

**MLA CITATION**

Sospeter, Maroa Dunstan & Catherine Ndungo. "Usawiri Chanya wa Hadhi ya Mwanamke katika Methali za Igikuria". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Jul. 2024, pp. 332-342, doi:10.37284/jammk.7.1.2048.

## UTANGULIZI

Methali ni hekima au falsafa ya watu wa kundi fulani (Svensson, 1994). Aidha, methali kama kipera cha Fasihi Simulizi ni sanaa ya namna ya kujieleza binadamu kwa njia ya kiufundi. Senkoro (1987, uk. 14) ameeleza sanaa kama kazi ya binadamu yenye mwigo wa uyakini uliofungamana na wakati, mazingira na mfumo wa jamii inayohusika. Sanaa ni kazi ya mikono na, au akili ya mtu, nayo aghalabu ina umbo dhahiri lenye maana na dhana maalum.

Fasihi ni sanaa kwa kuwa ni kazi ya akili ya binadamu yenye mwigo wa ukweli. Hata methali ni hivyo. Jambo linalotofautisha fasihi na aina nyingine za sanaa ni matumizi ya maneno (lugha) katika kujieleza. Kirumbi (1975, uk. 37) anadai kuwa sanaa ni kielelezo cha yaliyo moyoni na maadam lililo moyoni likitolewa nje limekusudiwa lijulikane.

Methali kama kipera cha fasihi simulizi ni sanaa maalum ielezayo masuala mbalimbali yanayothaminiwa na kulaaniwa katika jamii husika. Tangu zamani, ulimwengu umeendelea kushuhudia kuishi kwa pamoja na ushirikiano baina ya mwanamke na mwanaume katika matendo mbalimbali ya jamii ili kurahisisha maisha yao. Ni katika ushirikiano huo ambapo jamii imeendelea kuibua mitazamo tofauti kuhusu mwanamke na mwanaume jambo ambalo linadhihirika katika simulizi za jamii mbalimbali (Bennaars, 1995)

Lugha ni kifaa muhimu kinachosheheni thamani na mikatale ya jamii ambayo inaweza kumtukuza na kumdunisha mwanajamii yeyote yule. Hivyo, methali kama sehemu ya lugha hubeba falsafa mbalimbali za jamii ambazo zinapohakikiwa hudhihirisha hadhi ya watu katika jamii wanamoishi, (Maitaria, 1991). Ni katika msingi huu ambapo tumepania kuchunguza suala la usawiri chanya katika methali za Igikuria.

Tafiti ambazo zimewahi kufanywa katika kuchunguza nafasi ya mwanamke katika fasihi simulizi zinaegemea upande mmoja unaoonyesha kuwa mwanamke anadunishwa na kunyanyaswa na tamaduni nyingi za Kiafrika. Kwa mfano, Matteru (1993) na Ndungo (1998) wanadai kuwa fasihi simulizi inadunisha mwanamke. Lengo la Makala hii ni kuonyesha kuwa, ingawa kuna miktadha ya kijamii ambayo hupelekea mwanajamii yeyote kudunishwa, kuna baadhi yake ambayo hutoa nafasi kwa mtu kupokea sifa kulingana na matendo yake mema. Hivyo, kichocheo cha kuchunguza na kuchanganua usawiri chanya wa hadhi ya mwanamke katika methali za Igikuria.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2048

**Msingi wa Nadharia**

Nadharia ya Ufeministi ndiyo iliyoongoza utafiti huu. Ufeministi ni mkabala unaoangalia na kujaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii. Matatizo hayo yanasababishwa na jinsia yao. Hivyo, nadharia inayohusu masuala ya wanawake inajaribu kufichua matatizo yanayowapata wanawake kama tabaka la kiuchumi na vilevile kama wanawake (Njogu na Wafula, 2007).

Ufeministi ni dhana inayojumlisha mikabala ya kiuhakiki ambayo licha ya tofauti zake, inaelekea kukubaliana na kuafikiana kwenye masuala kadhaa na malengo yake ya kimsingi. Nadharia hii inaelezea msukumo na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kitamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi.(Njogu na Wafula 2007). Pingu ambazo zimejengeka kwenye misimamo na itikadi ya kiume.

Wahakiki wa Kifeministi kama Birke (1986) na Randall na Lovenduski (2004) wanasema kwamba, Ufeministi ni dhana inayoelezea hali ya tendo la wanawake wanaodai kujieleza katika jamii mbalimbali na wanaume wanaounga mkono jitihada za wanawake hao. Ni dhana inayopinga mfumo dume.

Wanawake wamepigania haki zao tangu jadi. Japo maandishi yanayoangazia hali zao yalianza katika karne ya kumi na tisa hasa wakati wanawake wa kimagharibi walianza kuzungumzia juu ya matatizo yao. Kazi za mwanzo kabisa za kifeministi ni; A *vindication of the rights of Women* (Wollstonecraft, 1992). *A Room of ones own* (Woolf, 2021). Kulingana na Wollstonecraft (Keshatajwa), mielekeo hasi kumhusu mwanamke imesababishwa na elimu mbovu wanayopewa wanawake na wanaume.

Chapisho lililochangia zaidi katika maendeleo ya uhakiki wa Kifeministi ni *The Second Sex* (1952) la mwandishi wa Kifaransa Beauvooir (1994). Mwandishi huyu kimsingi alikuwa akishambulia na kukosoa asasi zinazomnyanyasa mwanamke kama vile; dini, ndoa na utamaduni. Anasema kwamba, dini humkandamiza mwanamke kwa kumfanya kunyenyekea. Ndoa humfunga na kumfanya kuona uwezo wa mwanamume ilhali utamaduni humdunisha katika tamathali hasi.

Nadharia ya Ufeministi kama ilivyo katika fasihi ya Kiswahili ilizuliwa na Charles Fourier wa Ufaransa katika karne ya kumi na tisa akirejelea mwanamke aliyeazimia kubadilika na kubadilisha mitazamo ya jamii kumhusu (Ndungo, 1998). Hivi leo, mtazamo huu wa uchanganuzi unatumiwa kuchunguza mahusiano baina ya mwanaume na mwanamke katika jamii, asili yao na jinsi yanastahili kubadilishwa ili kuwanufaisha wote (Mitchel na Oakley, 1986) Mtafiti ametumia mtazamo huu katika kuchunguza uhusiano uliopo baina ya mwanamke na jamii yake (Wakuria) ili kudhihirisha hadhi chanya ya mwanamke kupitia methali za Igikuria

Ufeministi wa kifasihi ni mtazamo unaojifunga kwenye matini (mazungumzo na maandishi) ambao unasisitiza haja ya kutathmini na kuchunguza mahusiano ya watu (mke na mume) katika fasihi (Kolodny, 1986). Kwa mujibu wake, namna watu wanavyosawiriwa katika fasihi ndivyo hali ilivyo katika jamii halisi. Hivyo, ili kuelewa jamii fasihi yake ni muhimu kueleweka. Kuna watafiti wengi wa fasihi ambao wametumia mkondo huu wa uchanganuzi katika kueleza masuala ya kijinsia katika jamii kwa mfano Ndungo (1998) alitumia mkabala huu katika kuchunguza taswira ya mwanamke katika fasihi simulizi ya Kiafrika. Alichanganua methali za Wagikuyu na kubainisha kuwa mwanamke ana hadhi duni.

Tumetumia mkabala huu kudhihirisha usawiri wa hadhi chanya ya mwanamke katika methali za Igikuria. Mkabala huu umetufaa sana katika mada yetu kwa sababu tunatambua kuwa ili hadhi chanya ya mwanamke katika methali iweze kueleweka, fasihi simulizi ya jamii ya Wakuria ni sharti ichunguzwe na kueleweka. Fasihi simulizi kama asasi ya kijamii ya kuingiliana, husheheni falsafa mbalimbali za jamii zinazodhihirisha majukumu na hadhi za wanajamii. Hivyo, uchanganuzi wa methali za Igikuria ni muhimu katika kutambua sifa za mwanamke katika jamii ya Wakuria.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2048

Nadharia ya Ufeministi inadhihirisha sifa mbili kuu: Kwanza, utamaduni unatazamwa kama kifaa kinachomtwaza mwanamume huku kikimtweza mwanamke. Utamaduni huu unawarithisha wanajamii wake thamani hizo ambazo zinajitokeza kwenye sanaa ya lugha. Pili, utamaduni umeundwa kwa namna inayomkandamiza mwanamke katika nyanja zote za maisha. Makala hii kwa kiasi fulani inadhihirisha kinyume cha sifa hizo kwani ni za jumla sana.

Japo kuna mikondo tofauti ya mtazamo wa Ufeministi, kuna sifa bainifu za mtazamo huu. Ramazanoglu (1989), Wamitila (2002), Njogu na Wafula (2007) wameainisha sifa zifuatazo za nadharia ya Ufeministi:

- Ni nadharia inayonuia kusawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na uana, inapigania jamii mpya yenye msingi katika amali za kibinadamu. Baadhi ya amali ni za kike na za kijadi na ambazo zinadharauliwa katika jamii ya sasa.

- Inapendekeza mabadiliko licha ya vizingiti vinavyojitokeza katika jamii mbalimbali.

- Huazimia kubadilisha uhusiano wa kimenke kwa kuwapa wanawake nafasi ya kujitawala wenyewe kiuchumi, kisiasa na kisosholojia.

- Mikondo yote ya Ufeministi hudai kuwa mahusiano yaliyopo baina ya jinsia tofauti ambapo mwanamke amedhibitiwa na wanaume hayastahili. Ni sharti yabadilishwe.

- Ni nadharia inayotumia fasihi kama jukwaa la kueleza kwa uyakinifu hali inayomkumba mwanamke ili iweze kueleweka na watu wengi.

- Ni nadharia inayokuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa.

- Ni mtazamo unaojaribu kuhamasisha watumiaji wa sanaa wawe na wahusika wa kike ambao ni vielelezo wenye uwezo na wanaoweza kuigwa.

- Hatimaye, lengo muhimu la nadharia hii ni kuumbua na kuziweka wazi kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake na ambazo zimepuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanaume.

Japo mkabala huu ni muhimu katika kutetea masuala ya wanawake katika fasihi, unaegemea zaidi katika upande mmoja kuwa mwanamke ananyanyaswa. Hata hivyo, baadhi ya mihimili yake imetufaa katika uchanganuzi wa data. Uchanganuzi wa usawiri wa hadhi ya mwanamke katika methali za Igikuria utaegemea mihimili ifuatayo:

- Ni nadharia inayonuia kusawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na uana na inayopigania jamii mpya yenye msingi katika amali za kibinadamu. Baadhi ya amali ni za kike na za kijadi na ambazo zinadharauliwa katika jamii ya sasa.

- Mikondo yote ya Ufeministi hudai kuwa mahusiano yaliyopo baina ya jinsia tofauti ambapo mwanamke amedhibitiwa na wanaume hayastahili. Ni sharti yabadilishwe.

- Ni nadharia inayotumia fasihi kama jukwaa la kueleza kwa uyakinifu hali inayomkumba mwanamke ili iweze kueleweka na watu wengi.

- Ni mtazamo unaojaribu kuhamasisha watumiaji wa sanaa wawe na wahusika wa kike ambao ni vielelezo wenye uwezo na wanaoweza kuigwa.

Makala hii imechunguza na kuchanganua usawiri wa hadhi chanya ya mwanamke katika methali za Igikuria kwa lengo la kudhihirisha kuwa japo kuna madai kuwa mwanamke ananyanyaswa, kuna miktadha mingi katika jamii ambapo mwanamke hutambulika na kusifiwa kutokana na matendo yake mema.

**Mbinu za Utafiti**

Usampulishaji wa kimakusudi ulitumika ambapo eneo la Kehancha wilaya ya Kuria magharibi katika tarafa za Ikerege na Taranganya liliteuliwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2048

kutekeleza utafiti wetu. Eneo hili tulililoliteua linadhihirisha ule uasili wa utamaduni yaani bado halijavamiwa sana na tamaduni za kigeni au usasa kutokana na mwingiliano wa jamii tofauti zinazohama kutoka eneo moja hadi lingine.

Mbinu muhimu ya ukusanyaji wa data iliyotufaa ni ushirikishi wa watu binafsi wenye tajriba katika elimu na mila na desturi za jamii ya Wakuria. Hapa tuliteua wazee maalum tuliowahoji wakitujibu na kutoa maelezo zaidi kuhusu methali na dhana mbalimbali za maisha ya Wakuria. Ufafanuzi waliotupa tuliunakili kwenye kijitabu na kuurekodi kwenye kaseti kwa marejeleo ya baadaye. Aidha, tulitumia hojaji zenye maswali ya utafiti ambayo tuliwapa wanafunzi na walimu wa shule za tarafa ya Ikerege na Tarang’anya wakatusaidia kujibu maswali na kutoa maelezo zaidi ambayo tuliyachambua, tukayapanga na kuyachanganua kiusomi ili kukidhi mahitaji yetu.

Kulikuwa na haja kubwa vile vile ya kuwahoji baadhi ya wazee wenye tajriba ya maisha na utamaduni wa Wakuria ili kupata maoni yao juu ya fasihi simulizi ya Wakuria, utanzu wa methali pamoja na masuala yanayohusiana na utamaduni wao ili kutekeleza lengo letu barabara. Njia nyingine muhimu sana kwetu ilikua ni kutumia maktaba mbalimbali pamoja na vituo vya mambo ya kitamaduni kama vile; Kenya National Archives na Gosi Cultural Centre. Katika sehemu hizi tulipata fursa ya kusoma vitabu, majarida na makala mbalimbali yanayohusu methali na fasihi simulizi kwa jumla.

Katika uchanganuzi, tulichagua methali zinazotaja mwanamke moja kwa moja halafu tukazingatia zile zinazomtukuza. Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo na michoro faafu kwa kuzingatia lengo la utafiti na mihimili ya nadharia ya Ufeministi.

## MATOKEO NA MAJADILIANO YA MATOKEO

### Usawiri Chanya wa Mwanamke katika Methali za Igikuria

Usawiri chanya wa mwanamke kwa mujibu wa kitengo hiki, ni sifa zozote nzuri na zenye kusifu au kumpa pongezi mwanamke katika ujumbe utakaojitokeza kwenye methali mbalimbali tutakazozijadili. Nkwera (1979), Sengo (1985), Msokile (1992), Mulokozi (1996), Wamitila (2008) na Senkoro (2010) wanakubaliana kuwa, ujumbe ni miongoni mwa vipengele vinavyotokana na kipengele cha maudhui katika kazi ya fasihi.

Tumechanganua sampuli ndogo tu ya methali za Igikuria zinazomtukuza mwanamke. Utukufu huo unatokana na jinsi anavyoshiriki katika kuendeleza shughuli muhimu katika jamii yake. Baadhi ya methali zinazomtukuza mwanamke ni:

1. *Kaberre hai, Nyakongera angere mokari arrenge.*

(Mara mbili hapana, Nyakongera alikataa, ni mwanamke)

Methali hii ni sawa na ile ya Waswahili: **Kufanya kosa si kosa bali kurudia kosa.** Methali hiyo ya Igikuria ina maana kuwa kufanya kosa mara mbili ni vibaya. Katika jamii ya Wakuria, maovu yamelaaniwa tangu jadi. Nyakongera katika methali hii ni jina la mwanamke. Hatukupata kufahamishwa aliishi wapi na katika miaka ipi lakini inaaminika kuwa, alikuwa mtu mwenye umuhimu katika jamii ya Wakuria kutokana na jinsi alivyowaonya Wakuria dhidi ya kufanya matendo maovu. Nyakogera kama mwanamke, ni kielelezo bora katika jamii kwa namna anavyoadilisha watu wake na kutoa mafunzo yanayowafaa maishani. Hivyo, kupitia kwake tunatambua umuhimu alionao mwanamke kama **mshauri mkuu** ambaye akionya jamii kuhusu mambo fulani, inaitikia. Hadi leo huu msemo wa Nyakogera unatambulika na kuendelea kutumiwa ili kuonyesha umuhimu wa mwanamke katika shughuli mbalimbali za jamii ya Wakuria. Hadi sasa ushauri wa mwanamke ni muhimu katika masuala kama vile: uongozi, nyumba, siasa, sherehe za kitamaduni na shughuli nyingine muhimu katika jamii. Umuhimu wa ushauri wake hujitokeza zaidi katika malezi ya watoto na kuongoza jamii.

2. *Omokari, nkiaro gionswi.*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2048

(Mwanamke ni dunia)

Mwanamke katika jamii ya Wakuria ni nguzo muhimu katika kuendeleza kizazi cha jamii. Wazee tuliowahoji, mmoja wao mzee Mwita alitoa maelezo kuhusu methali hiyo kuwa:

> *"Wakuria wanamheshimu sana mwanamke kiasi kuwa pindi msichana anapozaliwa jamaa na marafiki wa wazazi hufurahia na kupiga vigelegele na nderemo (**kuchiira**) kama ishara ya kufurahia tendo jema la uzazi na kuwa kizazi kimeongezeka.*
>
> *Wakuria wanaamini kuwa msichana anapozaliwa huwa ameleta watu wengine au ameongezea ukoo kutokana na sababu kuwa baaadaye katika utu uzima ataolewa na kuendeleza kizazi cha jamii".*

Jukumu la mwanamke katika kuendeleza kizazi cha jamii ni la kimsingi sana. Mwanamke anapojifungua watoto huheshimiwa na kuletewa zawadi kemkem kama vile; mavazi, shanga, kuchinjiwa mbuzi au ng'ombe kama ishara ya pongezi katika kazi yake nzuri. Mbali na kuwa mwanamke ni msingi wa kuiendeleza jamii, pia ni mjenzi wa jamii kama inavyodhihirika katika methali ifuatayo:

3. *Omokari, mokora omigi.*

(Mwanamke ni mjenzi wa jamii)

Tangu jadi, mwanamke katika jamii ya Wakuria anatekeleza majukumu muhimu ya kuimarisha familia. Ujenzi tunaozungumzia hapa ni ule wa kuleta familia pamoja yaani: mume, mke na watoto na hata ukoo mzima. Wakuria wana imani kubwa kuwa mwanamke ni kiumbe mwenye huruma, mpole, asiye na wingi wa chuki, mwenye utu, mapenzi ya dhati na kadhalika. Sifa hizi zinampa nafasi kubwa katika kuleta jamii pamoja.

Wakuria, kama jamii nyingine za ulimwengu, wamepitia katika nyakati na vipindi tofauti vya kihistoria. Wakuria kama wafugaji walipata kushiriki katika vita na makabila jirani kutokana na mizozo ya wizi wa mifugo na mashamba. Hata katika kipindi cha vita vya pili vya ulimwengu, baadhi ya mashujaa wao (wanaume) waligura miji yao na kuishia msituni. Katika kipindi hicho, mwanamke ndiye aliyeachiwa jukumu la kulinda na kuikimu familia kwa kuipa mahitaji yale ya kimsingi kwa mfano; kulinda boma, mifugo, mashamba, mazao na kulea watoto kulingana na mila na desturi za jamii ya Wakuria.

4. Mugi *gotare mokari, niisara*

(Mji [au boma] usio na mwanamke ni chaka)

Umuhimu wa mwanamke katika jamii ya Wakuria unadhihirika katika jazanda iliopo katika methali hii. Senkoro (2018) anasema kuwa, matumizi ya sitiari ni miongoni mwa sifa muhimu katika kazi ya fasihi. Chaka ni kichaka kikubwa mfano wa msitu uliojaa miti, nyoka na wanyama hatari kiasi kuwa mtu aliye makini hawezi kuingiamo. Wakuria wanathamini na kuheshimu sana mwanamke kutokana na mchango alionao katika jamii. Majukumu ya mwanamke katika jamii ya Wakuria ni mengi mno. Mwanamke huielekeza jamii haswa vijana kupitia kwa mafunzo anayowapa tangu wakiwa watoto. Kina mama hutoa mafunzo haya kupitia kwa methali, nyimbo na tanzu nyingine za fasihi simulizi almuradi jamii nzima iweze kubadilika.

Kando na kutoa mafunzo kwa jamii, mwanamke ndiye anayefanikisha sherehe mbalimbali za kitamaduni kupitia kwa uongozi wake ulio makini, mapishi, nyimbo na kunadhifu mambo yote. Kutokana na umuhimu huo, inaaminika kuwa mji usiokuwa na mwanamke hauwezi kupokea wageni kwa njia inayofaa. Kutakua na dosari. Hata mwanaume anapokosa kuoa katika jamii ya Wakuria huchukuliwa kama aliyepotea na pindi afapo huwa jina lake linasahaulika kwa sababu uhifadhi wa majina ya wafu hufanikishwa kupitia kwa vizazi vidogo yaani watoto wanaozaliwa hupewa majina yao.

5. *Mokari agoseeta, nting'ana arong'aange*

(Mwanamke anayetafuta ni bora)

Methali hii inaweza kufasiliwa mara mbili. Kwanza, mwanamke kama mjasiliamali kwa namna ya kuitafutia aila yake riziki au utajiri wa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

kuikimu kupitia kwa shughuli za kilimo, ufugaji na kazi yoyote ya kuzalisha mali. Pili, kutafuta kwa njia ya uzazi yaani kupata watoto wengi ana umuhimu mkubwa. Katika jamii ya Wakuria, watoto ni muhimu sana. Watoto ndio utajiri wa Mkuria. Kawia (2015) anadai mwanamume mwenye wake wengi alihesabika kuwa tajiri, kwani, wanawake (na watoto) walitumika kama vitendea kazi. Namna mtu alivyo na watoto wengi ndivyo alivyo tajiri na hali kadhalika. Utajiri kupitia kwa watoto unatokana na falsafa kuwa mikono mingi hurahisisha kazi. Vijana wana umuhimu mkubwa katika kutekeleza kazi inayohitaji wingi wa watu kama vile; ukulima, ujenzi, ulinzi wa jamii dhidi ya adui na kadhalika. Aidha, watoto wanapofika umri mkubwa huoa na kupata nafasi ya kuendeleza kizazi cha jamii. Kutokana na ukweli huu, ni dhahiri kuwa mwanamke ana umuhimu mkubwa katika jamii ya Wakuria. Hivyo, jukumu lake la kiuzazi ndilo humpa nafasi na sifa kubwa. Mbali na kuwa mwanamke ni mjasiriamali, yeye ni mfadhili katika jamii yake kama ilivyo katika methali ifuatayo.

6. *Ibya musubati, mbiya karei.*

Vya dada (msichana) ni vya milele.

Methali hii ina maana kuwa vitu vinavyotoka kwa msichana aliyeolewa kwenda kwa wazazi wake au jamaa zake haviishi kamwe. Ukweli wa methali hii unajikita katika faida alizonazo msichana kwa aila yake. Faida ya msichana haina kipimo. Msichana katika jamii ya Wakuria ana umuhimu mkubwa ambao hauwezi kupuuzwa. Umuhimu wao unawafanya waonekane kama wafadhili katika jamii wanazotoka. Tangu kuzaliwa kwao wanatekeleza majukumu muhimu hasa yale ya kiuana katika jamii yao kama vile; kulima, kukusanya kuni, kuteka maji, kukandika nyumba na kadhalika. Pindi wanapotimia umri mpevu huozwa na hivyo kufanya jamaa zao kupata ukoo mpya, heshima, mali kupitia kwa mahari na zawadi nyingi hufululiza pasi kukoma.

Inaaminika kuwa hata binti aozwe na kuishi kwa mumewe miaka zaidi ya mia, zawadi huzidi kutoka katika familia hiyo kwenda kwa wazazi wake kwa miaka na mikaka. Kila upungufu unapotokea kwa wazazi wake, hasiti kutoa mchango wake. Mchango huu aghalabu hutolewa kwa njia ya mifugo hasa ng'ombe na nafaka. Aidha, nasaha na ushauri wake kuhusu mchakato wa maisha ya kila siku katika hizo familia mbili ni muhimu sana. Ufadhili wa msichana (mwanamke) ndio unaomfanya kuwa hai kwa wazazi na jamaa zake hata baada ya kuaga kwake, chambilecho; *Te musubati, akogota hai!*

7. *Te musubati, akogota hai.*

(Kina dada hawazeeki)

Watafitiwa waliweza kukubaliana na haya maelezo yaliyofafanua ujumbe wa hii methali kuwa kina dada huishi milele katika mioyo ya jamaa zao. Wakuria wanawatukuza mno binti wao kutokana na ukweli kuwa mchango wao katika shughuli nyingi za jamii si haba. Wasichana wa Wakuria hata baada ya kuolewa hawawezi kusahau aila yao. Wao huchangia kila wanapohitajika kufanya hivyo au wasipohitajika. Kwa mfano ndugu wao wa kiume wanapotaka kuoa huwa hawana budi kuchangia kwa kulipa mahari. Hata hii leo binti waliosomeshwa na kupata kazi huchangia kulipa karo ya wadogo wao, kuwajengea wazazi wao nyumba na kuchangia katika shughuli nyingine muhimu zinazohitaji msaada wao.

Kutokana na utendakazi wa mwanamke katika jamii ya Wakuria kuwa mpana, hawezi kusahaulika au kuzeeka kwa akili na mioyo miongoni mwa wanajamii. Methali nyingine yenye ukuruba na hii ni;

8. *Kereeyoe karai, nukueboa nkarei*

(Kinacholiwa kwa muda mrefu, kusahaulika pia huchukua muda)

Ingawa jina la mwanamke halijitokezi katika methali hii ya Wakuria, kimuktadha, ni methali inayoashiria wanawake. Ni methali inayoshadidia umuhimu wa mwanamke katika jamii. Mwanamke anadhihirishwa kama mfadhili mkubwa katika aila atokayo kutokana na ukweli kuwa yeye ndiye chemchemi ya vizazi vyote.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2048

Majukumu yake ni faida kubwa katika jamii iliyo na matumaini ya maisha ya baadaye. Mwanamke ndiye huleta watu wanaojenga utajiri wa jamii na pia kuwafaidi kupitia miktadha mbalimbali ya jamii kwa mfano kupitia kwa uzalishaji mali wa biashara, kilimo, ufugaji, mahari, uzazi na kadhalika. Kutokana na faida hizi zinazodumu kwa muda mrefu katika jamii yake, inawachukua watu muda mrefu kabla ya kusahau fadhila zake.

Kimsingi, faida ya mwanamke kama ilivyo kwa mtu yeyote inatokana na kazi muhimu zenye manufaa anazozitekeleza katika jamii yake. Zawadi zinazotolewa kwenda kwa familia yake kwa mfano huwa ni zile za milele. Faida hizi humfanya mwanamke kuwa hai hata baada ya vizazi vyake vingi kupita.

9. *Hano ensaacha yaabora, neenkari ekogogwa.*

(Ng'ombe wa kiume anapokosa wa kike ndiye anachinjwa)

Methali hii inatumika kijazanda kuashiria umuhimu wa mwanamke katika jamii ya Wakuria. Kwa kawaida, ng'ombe wana umuhimu mkubwa kwa Wakuria. Mbali na kuwa kiwakilishi cha utajiri wao, hutumika kulipa mahari, kukamuliwa maziwa, ngozi hutumiwa kwa malazi, kulima mashamba kwa kukokota jembe, kutolewa katika kafara za kidini na kuchinjwa katika sherehe mbalimbali za kitamaduni. Katika shughuli hizo zote, wale ng'ombe wa kiume (ndume) ni muhimu. Wao ndio huchinjwa kutokana na sababu kuwa, hawazai na hivyo basi inachukuliwa kuwa, hawaongezi idadi ya ng'ombe. Pale anapokosekana tu ndume ndipo ng'ombe wa kike huchinjwa kama hatua ya mwisho kwa sababu ng'ombe wa kike ana umuhimu mkubwa katika kuzaa na kutoa maziwa. Fasili ya jazanda iliyoko katika methali hii ni kuwa katika jamii ya Wakuria mwanamume anapokosekana katika shughuli muhimu ya jamii, mwanamke hutekeleza jukumu hilo. Hata katika boma, mwanamume anapoondoka kwa mfano labda kushiriki katika shughuli za mbali kama vile biashara au ufugaji, vita, anapoaga dunia, mwanamke huendeleza majukumu yote ya mumeo.

Methali hii haikusudii kuonyesha kuwa mwanamke huja nafasi ya pili baada ya mwanamume bali inasisitiza usawa uliopo kati ya mwanamke na mwanamume katika kutekeleza shughuli mbalimbali za jamii. Aidha, inaonyesha namna mwanamke alivyo na nafasi sawa ya kutekeleza majukumu yote yanayotekelezwa na mwanamume. Kwa mfano; kushiriki katika ujenzi wa boma, kulinda na kufuga mifugo, kutoa malezi bora kwa jamii, kulima mashamba, kushauri jamii na kadhalika. Hadi sasa jamii ya Wakuria inaheshimu mwanamke na kumpa nafasi ya kuongoza na kutenda yale yote ambayo yanaweza kuendeleza jamii kwa mfano, mwanamke huwa balozi katika vijiji na kushikilia nyadhifa kuu katika jamii na katika asasi za kiserikali. Methali nyingine yenye mawazo sawa na hii ni:

10. *Hano irreengo reruho, ensaragena ikaraho.*

(Mwamba uking'olewa jiwe (dogo) huchukuwa nafasi yake)

Methali hii ni jazanda. Irreengo ni mwamba au jiwe kubwa. Mwamba unapong'olewa kutoka mahali pake labda kwa shughuli za ujenzi, jiwe dogo ndilo hubakia au kuchukua nafasi yake. Kimuktadha, ni methali inayodhihirisha umuhimu wa mwanamke katika jamii ya Wakuria. Mwanamke kama kiongozi ana uwezo wa kutenda mambo yoyote yale ambayo mwanamume anaweza kutekeleza. Yeye huwa ana uamuzi kwa mambo yanayohusu watu wake wanaomtegemea na hata kwa jamii yote kwa jumla. Umuhimu unaotekelezwa na mwanamke katika jamii ya Wakuria unasisitizwa zaidi na methali ifuatayo:

11. *Eno (niriga) neeno etabooreyoe Mogendi, iga tiga gusuba (omokari neencheraare)*

(Hili (jambo) ni lile aliambiwa Mogendi kuwa acha kung'atuka (mkeo yu njiani)

Wakuria wanathamini sana sherehe. Kuna sherehe mbalimbali ambazo zinaadhimishwa katika jamii ya Wakuria kutokana na umuhimu zinaoutekeleza: kushirikisha jamii katika matendo

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2048

mbalimbali ya kitamaduni na kutoa nafasi kwa mwanajamii kufuzu kutoka kundi moja hadi jingine kwa mfano; mtoto alipozaliwa, sherehe za kuvuka utoto, sherehe za kuvuka ukapera na sherehe baada ya mtu kutimiza umri wa kung'atuka. Katika sherehe zote, mwanamke ni muhimu sana na bila yeye kuwepo, haziwezi kufanyika. Methali tunayoijadili hapa hutumiwa kuonyesha umuhimu wa mwanamke katika sherehe na shughuli zozote za jamii. Umuhimu wa mwanamke unashuhudiwa katika majukumu muhimu anayotekeleza katika sherehe yoyote ile. Yeye ni kiongozi wa shughuli mbalimbali katika sherehe, mshauri wa jamii kuhusu maandalizi, huamua mambo tofauti, ni malenga au manju na ndiye hukaribisha wageni na kurembesha hafla yote.

Hata Mogendi; katika kisa kimoja, alipotaka kuadhimisha sherehe yake ya uzeeni bila ya mkewe kuwepo, alikatazwa na sherehe hiyo haikufanyika kamwe! Hii ni hali inayodhihirisha jinsi mwanamke anavyotukuka katika jamii ya Wakuria. Tangu kipindi cha zamani hadi kufikia cha sasa, ni wazi kuwa, sherehe nyingi za kitamaduni au dini hujumuisha wanawake na haziwezi kufanyika bila uwepo wao.

12. *Omokari, mahocha matamwi*.

(Mwanamke hukuza (wanaume) wasio mwelekeo)

Maarifa aliyo nayo mwanamke humwezesha kuikimu jamii hata pale ambapo mwanamume anakaa kuzubaa, bidii ya mwanamke humwezesha kulisha jamii kutokana na juhudi za ukulima na ufugaji, almuradi familia iendelee. Kuna visa mbalimbali katika jamii ya Wakuria ambavyo vinadhihirisha namna wanawake wamezitunza familia zao kwa bidii yao hasa wakati waume wao wamezama katika ulevi na kurandaranda ovyo.

13. *Omokari, mborabu bu kumugi*.

(Mwanamke ni mwanga ulio kwenye boma)

Katika methali hii, mwanamke analinganishwa na mwangaza. Kijuu juu tulipata kuelezwa na mzee mmoja, Mwita, kuwa katika jamii ya Wakuria, wengi wa wanawake ni weupe. Hivyo, wanaume wengi wanaotaka kuoa wanawaendea wasichana weupe ili wawamulikie na kuangaza kwenye maboma yao. Mwanzoni tuliona kisa hiki kama kichekesho kumbe ni sitiari. Ujumbe uliomo katika methali hii ni dhihirisho la namna mwanamke alivyo na jukumu la kuelimisha jamii hasa watoto, vijana na wanajamii wengine. Aidha, wanawake wamepewa jukumu la kuondoa ujinga wa kutofahamu ndio maana wengi wao wanatekeleza kazi za ukunga na uganga zinazohitaji ujuzi mkubwa.

14. *Mokari anyumba, nchara etasiome*

(Mwanamke aliye nyumbani njaa haivizii)

Umuhimu wa mwanamke hapa unadhihirika katika malezi bora. Bidii ya mwanamke katika kutafutia familia yake riziki inazingatiwa. Kuna imani kubwa miongoni mwa Wakuria kuwa ni nadra sana njaa kuvizia nyumba iliyo na mwanamke kwani yeye huwa na kijishamba cha mboga. Vilevile, katika kila nyumba ya mwanamke hapawezi kukosekana chakula. Juhudi zake huwa ni muhimu katika kuiokoa jamii kutoka kwa hali ngumu kama vile; ukame na njaa.

15. *Omokari akumugi, nkioge ke mubisa.*

(Mwanamke aliye nyumbani ni silaha kwa adui)

Methali hii inasisitiza jukumu la mwanamke katika hali ya ulinzi na kuleta usalama nyumbani na kwa jamii nzima. Mwanamke analinganishwa na silaha dhidi ya adui kwa namna alivyo mwepesi wa kusikia adui na kuwafahamisha majirani kuhusu uvamizi wa ghafla. Kwa kuwa jamii ya Wakuria ni ya wakulima na wafugaji, mwanamke kila mara hata anapokuwa amelala huwa makini ili kusikia iwapo kuna adui nje ya boma. Kila anapotambua adui humwamsha mume na kupiga mayowe ili kuwapasha watu habari. Kwa hivyo, mwanamke ni silaha ya kuwinga adui na hivyo basi, huwa na jukumu la kiulinzi katika jamii. Katika jamii za Kiafrika, wanawake wengi walishiriki katika harakati za kupigania jamii zao enzi ya ukoloni kwa mfano Mekatilili wa Menza katika miaka ya 1984 huko Pwani, alipigania

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

uhuru wa Wapwani, mwanamazingira Wangari Mathai alipigana vita dhidi ya kukata, kuteketeza na kunyakua misitu na kadhalika.

Mifano ya methali tulizochanganua hapa zinadhihirisha utukufu wa mwanamke katika jamii ya Wakuria. Amesawiriwa kama mshauri mkuu, mwendelezi wa kizazi cha jamii, mjenzi, mshirikishi, mjasiliamali, kiongozi, mlezi, mfadhili, mlinzi miongoni mwa sifa nyingine. Tofauti na sifa tukufu tulizodhihirisha katika utafiti huu, Sengo (1977) alianisha vyeo tisa ambavyo vinampa mwanamke utukufu mkubwa mno; Ni mama, nani kama mama? Yeye ni dada, yupi asiyetiwa na kuthaminiwa na kaka zake wote? Yeye ni binti wa baba, kwamba ni mdogo wa mama wa baba? Yeye ni mke, Waziri mkuu wa ndoa zote? Yeye ni shangazi, baba wa kike. huku yuko kule, yeye ni nyanya, malkia dikteta wa uzawa. Yeye ni mkwe, mke wa mjomba. Yeye ni mamamkwe, ni shemeji. Tofauti na methali zinazomtukuza mwanamke, tulikumbana na zile zinazomdunisha na kumdhalalisha mwanamke pengine kutokana na mila na tamaduni mbovu na desturi hasi zilizopitwa na muda. Tulichanganua japo kwa kifupi methali tisa kwa lengo la kufanikisha utafiti huu.

Mtazamo wa Ufeministi ambao uliongoza katika uchanganuzi wa tasnifu hii umefanikisha utafiti huu kwa kuwa, baadhi ya mihimili yake kuu imejitokeza katika methali tulizozichanganua. Nadharia ya Ufemenisti wa kifasihi inapigania usawa wa kijinsia. Katika tasnifu hii, tuliazimia kuonyesha jinsi mwanamke katika jamii ya Wakuria alivyo na majukumu muhimu sawia na yale ya wanaume licha ya kufinyiliwa na utamaduni mbaya. Kuna methali zinazoonyesha majukumu ya kimsingi anayotekeleza mwanamke ambayo hutekelezwa na wanaume kwa mfano; *Eno (niriga) neeno etabooreyoe Mogendi, iga tiga gusuba omokari neencheraare (Hili (jambo) ni lile aliambiwa Mogendi kuwa acha kung'atuka (mkeo yu njiani), Hano ensaacha yaabora, neenkari ekogogwa. (Ng'ombe wa kiume anapokosa wa kike ndiye anachinjwa), Hano irreengo reruho, ensaragena ikaraho (Mwamba uking'olewa jiwe (dogo) huchukuwa nafasi yake)*

Katika mhimili wa tano wa nadharia ya Ufeministi, methali kama sehemu ya fasihi simulizi zimechanganuliwa ili kuonyesha hali halisi alimo mwanamke katika jamii ya Wakuria. Baadhi ya methali tulizojadili zimedhihirisha utukufu wa mwanamke na jinsi jamii inavyosherehekea matendo yake kwani manufaa anayoleta mwanamke katika jamii ni ya kudumu. Kwa mfano: *Te musubati, akogota hai.* (*Kina dada hawazeeki)* na *Ibya musubati, mbiya karei (Vya kina dada (msichana) ni vya milele).*

Aidha, katika mhimili wa saba wa nadharia ya ufemenisti inapendekeza wahusika wa kike vielelezo. Utafiti huu umechanganua methali za Igikuria ambazo zinamtukuza mwanamke. Kuna methali kadhaa ambazo zimeonyesha sifa nzuri za wanawake kutokana na matendo mema wanayoshiriki katika shughuli za jamii. Wao ni kielelezo cha kuigwa na jamii nzima. **Nyakogera** katika; *Kaberre hai, Nyakogera angere mokari arrenge. (Mara mbili hapana, Nyakogera alikataa, ni mwanamke*) ni kielelezo mwafaka wa mhusika wa kike aliyetekeleza uongozi bora katika jamii ya Wakuria. Dhana ya wanawake kuwa viongozi bora pia imeonekana katika methali: *Omokari, mahocha matamwi* (*Mwanamke hukuza (wanaume) wasio mwelekeo*) na *Hano ensaacha yaabora, neenkari ekogogwa* (*Ng'ombe wa kiume anapokosa wa kike ndiye anachinjwa*).

## HITIMISHO

Katika makala hii tumechunguza na kuchanganua usawiri wa utukufu wa mwanamke katika methali za Igikuria. Methali tulizochunguza na kuzieleza sio zote. Tulifafanua tu baadhi ili kutoa ushahidi kuwa mwanaume na mwanamke wametukuka katika jamii ya Wakuria. Utukufu huo unatokana na mchango wake katika shughuli muhimu anazoshiriki katika jamii. Katika methali za Igikuria mwanamke amesawiriwa kwa namna inayomletea utukufu. Anajitokeza kama; kiongozi wa shughuli muhimu, mpatanishi, mshirikishi, mjenga uchumi, mshauri mkuu, mfadhili, mlezi wa watoto na jamii, mlinzi, mwendeleza jamii, mkuza uchumi na kadhalika.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2048

**MAREJELEO**

Beauvoir, S. (1994). *The Second Sex*. London: Jonathan cape.

Bennaars, G. A. (1995). Gender Education and the Pedagogy of Difference: The African predicament. In *Basic Education Forum* (Vol. 6, Uk. 23-34).

Birke, L. (1986). *Women Feminist and Biology. The Feminist Challenge*. Wheatsheal: Collins.

Kirumbi, P. S. (1975). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Shungwaya Publishers L.T.D.

Kolodny, A. (1986). Dancing through the minefield: some observations on the theory, practice and politics of a feminist literary criticism. Feminist studies, 6(1), Uk. 1-25.

Lovenduski., & Randall, V., &, J. (2004). Gender in contemporary British politics. The British Journal of Politics and International Relations, 6(1), 1-2.

Maitaria, J. N. (1991). *Methali za Kiswahili kama chombo cha Mawasiliano; Mtazamo Wa Kiismu-Jamii*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. Kenyatta University Institutional Repository. (Haijachapishwa).

Matteru, M. L. B. (1993). *Fasihi Simulizi na Uandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mitchell, J. na Oakley, A. (1986). *What is Feminism*. Oxford: Basil Blackwell.

Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Kibaha: Education Publishers and distributors ltd.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Ndungo, C (1998). *Images of Women in African Oral Literature; Acase of Gikuyu and Swahili Proverbs*. Unpublished PHD Thesis, Kenyatta University. Kenyatta University Institutional Repository.

Njogu, K. na Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkwera, F. V. (1979). *Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyuo* (Vol. 4). Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Ramazanoglu, C. (1989). *Feminism and The Contradictions of Oppression*. London: Routledge.

Sengo, T. S. Y. (1985). *The Indian Ocean Complex and the Kiswahili Folklore: The Case of the Zanzibarian Tale-Performance*. Unpublished PhD Thesis, University of Khartoum. University of Khartoom Institutional Repository.

Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na jamii*. Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (2010). Kiswahili Literary Portrayal of Gender and Migration in Africa: An African Perspective? In *Unpublished paper presented at Codesria Gender Symposium, Cairo, Egypt, November* (Uk. 24-26).

Svensson, A. (1994). *Ibiirengio*. Nairobi: Phoenix Publishing House.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Phoenix Publishers L.T.D.

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Focus Books.

Wollstonecraft, M. (1992). A Vindication of the Rights of Woman. 1792. *The Works of Mary Wollstonecraft*, *5*, 217.

Woolf, V. (2021). *A Room of One's Own*. Virginia: Global Grey.

Woolf, V. (1929). Feminism, Women, literature, education. London: Hogarth Press.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.